BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 18 Septemba, 2026**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Kazi na Uwekezaji:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo.

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake.

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

75. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Miongoni mwa ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ni kupatiwa ajira wahudumu wa Afya ya Jamii wanaofanya shughuli zao katika maeneo ya vijijini.

    Je, mpango huu umefikia hatua gani katika utekelezaji wake.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

196. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Taarifa za utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) hutoa fursa ya kubaini changamoto na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

    (a) Je, Zanzibar imenufaika vipi na fursa hizo.

    (b) Je, ni msaada gani wa kitaalamu na kifedha uliopatikana kwa ajili ya kuimarisha haki na huduma za Watu Wenye Ulemavu, uliotokana na taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

290. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Wananchi wanalalamikia kuongezeka kwa kesi za udhalilishaji, huku baadhi ya kesi zikichukua muda mrefu kukamilika, licha ya juhudi zinazofanywa na vituo mbalimbali pamoja na jamii katika kuripoti na kufuatilia matukio hayo.

    (a) Je, Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, inaeleza nini kuhusu ucheleweshaji wa uendeshaji na ukamilishaji wa kesi za udhalilishaji.

(b) Ni kesi ngapi za udhalilishaji zimefikishwa katika Ofisi hiyo katika miaka mitatu iliyopita, na ni ngapi zimekamilika.

(c) Ni hatua gani zinazochukuliwa kuharakisha kesi hizo bila ya kuathiri haki za waathirika na watuhumiwa.

291. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ucheleweshaji wa upelelezi, uendeshaji wa mashtaka na kukamilika kwa mashauri, kunasababisha baadhi ya wananchi kusubiri haki kwa muda mrefu na kuongeza mrundikano wa kesi katika mfumo wa utoaji haki.

(a) Je, Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ina mkakati gani wa kupunguza mrundikano na ucheleweshaji wa mashauri ya jinai.

(b) Je, ni mashauri mangapi yaliyopo ambayo yamesubiri kukamilika kwa zaidi ya mwaka mmoja, na sababu kuu za ucheleweshaji huo ni zipi.

(c) Je, ni hatua gani za pamoja zinazochukuliwa na Ofisi hiyo pamoja na taasisi nyingine katika mnyororo wa haki, ili kupunguza muda wa kushughulikia mashauri.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

174. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa Manispaa ya Wete na Chake Chake zina changamoto ya kutokuwa na gari za kutosha za kubebea taka, jambo linalofanya shughuli za usafi kuwa ngumu.

Je, lini Serikali itaipatia ufumbuzi changamoto hii ya gari kwa kuwanunulia gari la kusombea taka katika Manispaa hizo.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

8. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

   Ujenzi wa Viwanja vya Michezo kwa maeneo ya Wilaya za Zanzibar, ni mradi uliogubikwa na changamoto nyingi pamoja na kutoridhisha utekelezaji wake.

   (a) Ni viwanja vingapi hadi sasa vimeshajengwa kwa Unguja na Pemba na kwa gharama za kiasi gani.

   (b) Ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na kuchelewa kukamilika pamoja na kutokutimia kwa vigezo na viwango vya kiwanja cha Ukutini Pemba.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

228. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

   Katika maeneo ya Bonde la Mzungu yanayotumika kwa kilimo, kulitokea uvamizi wa uuzaji wa viwanja.

   Ni hatua zipi Serikali imechukua kuzuwia uvamizi na hatua gani zilizochukuliwa kwa wale waliovamia katika maeneo hayo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

277. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

   Kumekuwa na matukio ya wananchi kupoteza maisha kutokana na shoti za umeme pamoja na kuungua kwa nyumba na makaazi ya wanafunzi, hali inayoibua wasiwasi kuhusu usalama wa miundombinu na mifumo ya umeme.

   (a) Je, Serikali kupitia Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), ina mpango gani wa kupunguza vifo, majeruhi na uharibifu wa mali unaotokana na hitilafu za umeme.

   (b) Je, uchunguzi gani umefanyika kubaini sababu za matukio ya shoti za umeme na moto katika maeneo yaliyoathirika.

(c) Je, hatua gani za kiusalama zimechukuliwa kuzuia matukio kama hayo kujirudia.

**Wizara ya Afya:**

165. MHESHIMIWA MASOUD AMOUR MASOUD (Jimbo la Amani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Je, mchakato wa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wananchi kusajiliwa na kupatiwa kadi za ZHSF umefikia hatua gani.

(b) Ni lini zoezi hili litakamilika ili wananchi waendelee kufaidika na huduma za afya kwa hospitali za Serikali na binafsi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

137. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Watembezaji Watalii *(Tour Operators)* wanaokwenda kwenye fungu la mchanga linalojulikana kama “Nakupenda *Sand Bank*” hutozwa fedha. Vile vile, kumekuwa na umwagaji wa taka nyingi kwa vyombo vinavyopeleka Watalii katika eneo hilo, na kuhatarisha mazingira na viumbe vya baharini.

Je, kwa nini Wizara imekosa kuweka na kusimamia miongozo ya wanaokwenda eneo hilo dhidi ya umwagaji taka ovyo.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

88. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na uchukuzi:

Serikali inatekeleza Mradi wa Bandari ya Maruhubi kwa kupitia mfumo wa ubia wa mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Binafsi (Public Private Partnership (PPP)).

(a) Serikali ina wajibu gani wa kifedha katika utekelezaji wa Mradi wa Bandari ya Maruhubi.

(b) Je, Serikali inapata mgawanyo gani wa mapato kupitia Mradi huu wa Bandari ya Maruhubi.

(c) Je, kuna mpango gani mbadala ambao utahakikisha utekelezaji mzuri wa mradi huu, ili kuepusha kasuasua kwake hapo baadae.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

43. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekeza kwa kiwango kikubwa katika kilimo cha kahawa katika shamba la Kizimbani, kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na kupanua vyanzo vya mapato ya Taifa.

(a) Je, uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Shamba la Kahawa la Kizimbani, umeleta tija gani hadi sasa.

(b) Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuendeleza kilimo cha kahawa, ili zao hilo liweze kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa wananchi.

## Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

189. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Je, Serikali kwa sasa ina mifumo mingapi ambayo usimamizi, matengenezo, uendelezaji (System Enhancement) na huduma za msaada wa kiufundi (Technical Support) bado zinategemea ‘vendors’.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

34. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Kwa kuwa hivi sasa Serikali ya Awamu ya Nane inafanyakazi nzuri sana ya kuimarisha miundombinu katika sekta mbalimbali za Ustawi wa Jamii, Usafirishaji na Uwekezaji. Na kwa kuwa kazi hizo zimewezesha makampuni kadhaa ya ujenzi kuja kufanyakazi ambazo nyengine zinahitaji wataalamu mahususi na nyengine hazihitaji wataalamu mahususi na mtu anaweza kupata uzoefu akiwa kazini moja kwa moja.

(a) Je, ni ajira ngapi zisizohitaji utaalamu mahususi zimepatikana kwa Vijana wa Zanzibar kupitia Kampuni zinazotekeleza miradi ya maendeleo.

(b) Je, ni ajira ngapi zinazohitaji utaalamu mahususi zimepatikana kwa Vijana wa Zanzibar kupitia Kampuni zinazotekeleza miradi ya maendeleo.

(c) Je, kuna makubaliano gani hufanyika kwa wenye makampuni hayo kuweka asilimia fulani ya ajira kwa vijana wa Zanzibar hasa kwenye maeneo ambayo miradi hiyo huwa inafanyika.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Kazi na Uwekezaji:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake - Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

**<u>Waziri wa Fedha na Mipango:</u>**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Zanzibar,
18 Septemba, 2026.

(Ramadhan Khamis Juma)
KAIMU KATIBU WA BARAZA LA
<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>